KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na Derek Morris – Raisi ya *Hope Channel International*

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la 8, Mei 15 – 21, 2020

KUBADILISHWA NA UPENDO WA MUNGU

Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu. Yeremia 31:3

Mary Ann Roberts alikulia katika nyumba ya Kikristo, lakini akiwa kijana, hakujitoa binafsi kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yake. Baada ya kuhitimu chuo aliolewa, mume wake alijiunga na jeshi, na wakahamia Ulaya. Ilikuwa ni kule Ulaya ambako Mary Ann aliacha mambo yote yaliyomwunganisha na kanisa na akageuka kuishi maisha ya kidunia.

Mnamo mwaka 1983 aligonga mwamba. Katikati ya maburudisho ya siku za mapumziko za mwisho wa juma yaliyoambatana na unywaji pombe, alilewa mno na akawa mgojwa kiasi cha kushindwa kuungana na familia yake. Ndipo Mary Ann alipoamua kumwomba Mungu amrudie maishani mwake. Picha wazi iliyomjia akilini mwake wakati ule akiwa katika hatua duni ya maisha yake ilikuwa ni ya Baba anayekimbia barabarani kwenda kukutana na Mwanae Mpotevu. Mary Ann alijua kuwa yeye ndiye yule mtoto.

Huku akitambua kuwa ilimpasa kufanya mabadiliko makubwa katika mtindo wake wa msisha, alimwandikia barua mchungaji wa Kikristo na kumwambia kuhusu kujitoa kuwa mfuasi wa Yesu.

Mke wa mchungaji alielewa ugumu ambao Mary Ann angeupata katika kipindi cha mabadiliko na akamwunga mkono kwa kuomba naye kwa njia ya simu kila siku asubuhi kwa mwaka mzima.

Hata baada ya Mary Ann kuanza kuhudhuria kanisani na kumfanya Mungu kuwa sehemu muhimu ya maisha yake, alihisi kuwa kuna kitu fulani kilikuwa kinakosekana – kwamba Mungu alikuwa amemtunzia kitu fulani cha pekee ambacho bado alikuwa hajakigundua. Daima alikuwa anatamani kama angeendeleza elimu yake, na akaamua kurudi tena shuleni. Alidhani kuwa yumkini hilo lingeweza kuziba pengo moyoni mwake. Alipeleka maombi na akakubaliwa katika programu ya elimu ya juu na hatimaye alikamilisha kwa kupata shahada ya Uzamivu (Phd) katika fani ya sayansi ya mfumo wa fahamu. Lakini kwa namna fulani maisha yalionekana kama bado hayajakamilika.

Mnamo msimu wa kiangazi wa mwaka 2001, Mary Ann alihudhuria mkutano wa makambi kule North Carolina. Alivutiwa zaidi kujumuika na marafiki, kwa hiyo alikaa karibu na mwisho wa ukumbi kwa nyuma. Katika moja ya vipindi alimsikia mwinjilisti mmoja wa Kikristo akiwaalika wale waliokuwa wanavutiwa kwenda Kenya kwenye mradi wa huduma ya utume, wakutane naye baada ya ibada.

“Kwa kawaida huwa napenda kutafakari mambo kabla ya kuchukua hatua,” Mary Ann anakumbuka, “lakini ilikuwa ni kana kwamba kuna mtu amesimama mbele yangu na akionesha kunilenga moja kwa moja.” Mkutano ulipokuwa ukifungwa alitembea hadi mbele ya ukumbi akiwa na uthibitisho wa kina kwamba Mungu alikuwa anamwita kushiriki katika mradi wa huduma ya utume kule Kenya. Baadaya kuongea na Mary Ann, mwinjilisti alimwalika kuendesha mfululizo wa mikutano katika jamii iliyonyuma sana iitwayo Rongo, nchini Kenya. Mary Ann hakuwa mhubiri wa hadhara. Hakupata mafunzo ya kuhubiri na hakuwa na uzoefu kabisa wa kazi ya utume ya mstari wa mbele. Haikuwahi kuingia akilini mwake kwamba Mungu angemtaka awe mhubiri. Siku ile Mungu alikuwa wazi kuruhusu utendaji wa Roho

Mtakatifu, na kwa maneno yake alianza kuomba: “Bwana, ninakuruhusu unitupe kwenye mavuno yako.”

Miezi michache ilifuata na Mary Ann alisafiri kwenda Kenya kwenda kufanya kile Mungu alichomwita kufanya. Ingawa alikuwa na hofu, kila jioni aliposimama kuhubiri, alihisi Mungu akiongea na umati wa watu waliokusanyika kwenye uwanja wa mji kupitia kwake. Mwishoni mwa mkutano zaidi ya watu 500 walikiri upendo wao kwa Yesu kwa njia ya ubatizo. Mary Ann alijawa na furaha – furaha kuu! Na furaha ile haijatoweka. Mary Ann amekuwa akiendelea kuhubiri, kueneza upendo wa Mungu, na kufuata uongozi wake. Aligundua wito wake alipomruhusu Mungu amtumie kwenye mavuno yake.

Je! Utamruhusu Mungu akutumie katika mavuno yake? Inaweza isifanane na ilivyokuwa miezi mitatu iliyopita kabla zahama ya COVID-19 haijapiga. Lakini bado kuna mambo mengi ya kufanya, na roho nyingi zikisubiri kusikia habari njema! Omba na umwulize angetaka ufanye nini!

Maswali ya Moyoni: Vipi kuhusu maisha yetu leo? Tumemruhusu Mungu atutumie kwenye mavuno yake? Ikiwa tunajisikia tuko mbali na Mungu, hebu tukumbuke kuwa anatusubiri akiwa amekunjua mikono yake ya upendo kwa ajili yetu ili tumgeukie. Sio tu anataka kutukaribisha nyumbani, bali pia anayo sehemu ya huduma kwa ajili ya kila mmoja wetu. Je! Utaufungua moyo wako kwa wito wake?

Changamoto ya Moyoni: Tazama kote kukuzunguka uone njia tofauti ambazo kwazo Mungu anakuonesha upendo wake. Huenda utauona upendo wake kupitia watu wengine, kupitia viumbe, au kwa njia zingine. Unapogundua upendo wake kwa njia ya pekee, andika, kisha washirikishe watu wawili juma hili ukidai ahadi ya Yohana 15:12. Ifanye kuwa tabia yako kutafuta upendo wa Mungu na kwa njia za pekee uweze kushiriki upendo wake pamoja na wengine.

“Baba anatupenda, sio kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali alitupatia upatanisho kwa sababu anatupenda. Kristo alikuwa ndiye wakala, ambaye kupitia kwake, Mungu aliweza kumimina upendo wake usio na kikomo kwa ulimwengu ulioanguka. ‘Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake*.’ 2 Kor. 5:19. . .Upendo kama huo hauna cha kuulinganisha. Watoto wa mfalme wa mbinguni! Upendo wa Mungu usiona kifani kwa ulimwengu ambao haukumpenda!”* – Steps to Christ, p. 13, 15

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:

- Ellen White, *Steps to Christ,* chapter 1, “God’s Love for Man”
- Derek J. Morris, *The Radical Prayer*

Siku ya 50, Ijumaa, Mei 15, 2020

Taarifa ya Sifa:

- Elizabeth, W., anasema: “Ninamsifu Mungu kwa uweza wake wa uponyaji!”
- Mshiriki wa Uingereza, anasema: “Ninamsifu Mungu kwa kusikia maombi na kunipatia chakula na msaada wa kifedha kimuujiza kwa wakati mwafaka.
- Wanasayansi wanafanya kazi kwa shauku kutafuta chanjo na kinga zitakazosaidia kupunguza kasi ya kirusi. Jitihada nyingi zimefanywa na kuna matumaini!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** moyo ulio tayari kutumiwa na Mungu wakati wo wote na mahali po pote anapotuita
- **Ombea** uinjilisti wote kwa njia ya mtandao na shughuli za kanisa za kidijitali ili tuzitumie na zibarikiwe
- **Ombea** vijana ambao wapo kwenye bonde la kukata maneno kumpokea au kumwacha Kristo. Omba kwamba wauone upendo na ukweli wa Yesu na wamtumikie kwa furaha maisha yao yote.
- **Ombea** makundi mengi ya kanisa ulimwenguni yasiyo na makanisa ya kukutania na yanatafuta ardhi. Omba pia ili Mungu awaamshe washiriki wote ili washiriki katika shughuli za kuanzisha makanisa.

Siku ya 51, Jumamosi, Mei 16, 2020

MUNGU ANAVYOJITOA

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi – Warumi 5:8

"Mara tu dhambi ilipokuwepo, Mwokozi alikuwepo. Kristo alijua kuwa angeteseka, lakini bado alikuwa mbadala wa mwanadamu. Mara tu Adamu alipotenda dhambi, Mwana wa Mungu alijitokeza kama dhamana kwa jamii ya wanadamu." – In Heavenly Places, 13.2

Maswali ya Moyoni: Adamu na Hawa walipotenda dhambi, alikuwa ni Mungu ambaye, pamoja na kukataliwa na dhambi kutendwa dhidi yake, alichukua hatua ya kwanza kuuelekea ubinadamu. Alikuwa na mtazamo wa neema, msamaha, pamoja na ahadi, kwamba Yesu atamponda yule nyoka Shetani (Mwanzo 3:15) na kuwa kafara kwa ajili ya wokovu wao. Kristo angali akitembea kukuelekea wewe akiwa na mtazamo ule ule. Amejitoa kwako na kwa wokovu wako. Je! Utaikimbilia leo mikono yake ya upendo na kuikubali damu yake itakasayo na haki yake?

Taarifa ya Sifa:

- Dr. Hammel, (Daktari wa Tiba kule Berrien Springs) amepona ugonjwa wa Covid-19 baada ya maombezi ya jumuia ya waamini.
- Kanisa nchini China linaendelea kustawi ingawa kuna masharti ya Covid-19 na ukomunisti. Mamia ya maelfu wameunganishwa kwa njia ya mtandao kwa ajili ya ibada.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** Mungu afungue macho yako ili uone upendo wake usio na kikomo kwako. Mwombe akuoneshe zaidi tabia yake ya upendo kila siku.
- **Ombea** washiriki wa kanisa na viongozi kule Indonesia ambapo wengine waliambukizwa Covid-19 na wamefariki dunia.
- **Ombea** Papua New Guinea kama nchi haina vifaa vya kutosha katika kuhimili mripuko wa Covid-19.

Siku ya 52, Jumapili, Mei 17, 2020

KUJITOA KWA YESU

Haruni akawaambia maneno yote Bwana aliyonena na Musa akazifanya zile ishara mbele ya watu. Watu wakaamini, na waliposikia ya kuwa Bwana amewajilia wana wa Israeli, na ya kuwa ameyaona mateso yao, wakainama vichwa vyao wakasujudu – Kutoka 4:30, 31

Unatamani kujitoa kwake, lakini u dhaifu katika nguvu ya kimaadili, umo katika utumwa wa mashaka, na unadhibitiwa na tabia za maisha yako ya dhambi. Ahadi zako na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Utambuzi wa ahadi zako zilizovunjika na nadhiri zilizopotea unadhoofisha ujasiri wako katika uadilifu wako, na unakusababishia kujisikia kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini haikupasi kukata tamaa. Unachotakiwa kuelewa ni ule msukumo wa kweli wa nia. Hiyo ndio nguvu inayotawala asili ya mwanadamu, nguvu ya maamuzi, au ya uchaguzi. Kila jambo linategemea hatua sahihi ya nia. Mungu amewapatia wanadamu nguvu ya uchaguzi; ni juu yao kuitumia. Huwezi kuubadilisha moyo wako, wewe mwenyewe kumpatia Mungu mapenzi (ya moyo wako); lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpatia nia yako; kisha atatenda kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema. Hivyo, asili yako yote italetwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; kiini cha mapenzi yako kitakuwa ni yeye; mawazo yako yatakuwa katika mwafaka pamoja naye." – Steps to Christ, 47

Maswali ya Moyoni: Waisraeli walipokabiliana na ukweli wa ahadi ya Mungu ya upendo na wokovu toka kwenye utumwa, mwitikio wao ulikuwa ni kujisalimisha, kujitoa na ibada. Unapotafakari upendo wa ajabu wa Mungu kwako, unaweza kuchagua leo kuitikia kwa mtazamo sawa sawa na huo? Je! Utampa nia yako, maisha yako, na moyo wako? Mungu ni mwema. Anatamani kusaidia na kuponya. Wakati mwingine mchakato unaweza kuumiza, lakini una matokeo ya thamani. Kwa nini usiuache ulimwengu, ujisalimishe, na kutoa maisha na nia yako kwa Mungu leo na kamwabudu?

Taarifa ya Sifa:

- Masharti ya Covid-19 yamepelekea ongezeko la watu kupenda injili kule Mashariki ya Kati. Watu kadhaa, ingawa hawajulikani wamejiunganisha na kanisa kwa njia ya mtandao.
- Vuguvugu zito la maombi linaendelea katika Divisheni ya Kati mwa Amerika

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** Wainjilisti wa Vitabu ulimwenguni kote ambao wameathirika kutokana na janga hili. Omba kwa ajili ya njia zitakazofanya vitabu vyetu viweze kusambaa wakati huu na kwa wengi kubarikiwa wanapovisoma.
- **Ombea** wale washiriki waaminifu wanaotoa huduma kwa kutumia akiba ya chakula wakati huu. Waombee ili walindwe dhidi ya kirusi wanapoendelea kutoa huduma ya upendo katika jumuiya zao.
- **Ombea** walei, watendakazi wa Biblia, na wainjilisti wanaotegemea kilimo na shughuli zingine za kujitegemea katika kujikimu pamoja na familia zao. Ombea wale wanaoishi na kuhudumu kwenye maeneo yaliyoathirika kwa ukame mzito.

Siku ya 53, Jumatatu, Mei 18, 2020

KUJITOA KWA AJILI YA MARAFIKI

Ajifanyiaye rafiki wengi ni kwa uangamivu wake mwenyewe; Lakini yuko rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu. - Mithali 18:24

"*Yonathani, kwa kuzaliwa alikuwa mrithi wa ufalme, lakini alijua kuwa amewekwa kando kwa amri ya Mungu; kwa ajili ya mpinzani wake rafiki mpole na mwaminifu kuliko wote, aliyakinga maisha ya Daudi kwa uangamivu wake mwenyewe;... jina la Yonathani linathaminiwa mbinguni, na linasimama duniani kama shahidi wa uwepo na nguvu wa upendo usio na ubinafsi.* – Education, 157

Maswali ya Moyoni: Urafiki wa Yonathani na Daudi ulikuwa na ubora wa kiroho na kina ambacho hakionekani hata kwa uchache. Msingi wa urafiki wao ulikuwa ni agano takatifu la kusaidiana kiroho baina yao na kujitoa. Je! Unao marafiki wa kiroho? Je! Wewe ni rafiki wa kiroho wa mtu fulani? Kwa nini usichague kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya kiroho ya rafiki zako kwa kuweka kando tamaa na raha zako binafsi, na kutoa muda na upendo wako kuwasaidia rafiki zako katika kutembea kwao na Kristo?

Taarifa za Sifa:

- Mikutano ya injili inayoendeshwa na huduma ya *It is Written* kwa njia ya mtandao inaleta matokeo ya kushangaza ambapo maelfu ya watu wanahudhuria na wengi wanafanya uamuzi kumpokea Yesu. Watafutaji ukweli wanajiunga na makanisa mahalia ya Kiadventista kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Watu wengi ambao zamani walikuwa washiriki wa Kanisa la Waadventista wanajiunga na kanisa, asante kwa ongezeko la shughuli za ushuhudiaji kwa njia ya mtandao.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kwa jili ya marafiki zako, na hasa wale wasiomjua Kristo au waliopotea katika njia zao. Omba kwamba Mungu akupatie moyo wa kuwa na mvuto wa kiroho ulio chanya na makini katika maisha yao.
- **Omba** kwa ajili ya mikutano ya injili iliyopangwa kufanyika kule Rift Valley, Kenya, eneo ambalo halijaingiwa na kanisa letu.
- **Omba** kwa ajili ya kituo cha huduma za jamii cha Kanisa la Waadventista wa Sabato liitwalo Phoenix Beacon Light wakati washiriki wapya wakikiandaa ili kianze kuhudumia jamii yao.

Siku ya 54, Jumanne, Mei 19, 2020

KUJITOA KWA MWENZI /FAMILIA YAKO

Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana. – Waefeso 5:22, 25; 6:1, 4

Kinachosababisha mgawanyiko na ugomvi katika familia na ndani ya kanisa ni kujitenga na Kristo. Kumkaribia Kristo ni kukaribiana kila mmoja na mwenzake. Siri ya umoja wa kweli ndani ya kanisa na katika familia sio diplomasia, sio usimamizi, sio juhudi za mtu asiye wa kawaida za kushinda magumu – ingawa mengi ya hayo yatahitajika – lakini ni mwunganiko na Kristo." do—but union with Christ." – The Adventist Home, 179

Maswali ya Moyoni: Mwenzi wako na familia yako ni watu ambao maishani mwako unao wajibu makini; Kuwapenda, kuwasaidia, na kuwafundisha katika uhusiano wa furaha na upendo pamoja na Yesu. Je! Leo utajitoa ili kuwapatia rehema, msamaha, na upendo sawa na aliotoa Yesu kwako, kwa mwenzi wako na kwa familia yako? Je! Ni shauku yako kuwa kiongozi wa kiroho kwa ajili ya nyumba ayako? Mwombe Yesu leo aweze kutembea na wewe kwa kina na mwunganiko pamoja naye ili uweze kumuakisi vema kwa mwenzi na kwa familia yako.

Taarifa za Sifa:

- Prosper, O., anasema, "Ndiyo! Haijalishi kuna COVID-19, nitadumu kuimba sifa kwa Bwana Aliye Juu."
- Jon, W., anasema, "Zahama hii imenipatia shauku mpya ya kutembea na Kristo kwa karibu zaidi!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Mwombee** mwenzi wako, wazazi, watoto, ndugu zako, na wanafamilia wengine. Waombee ili wamjue Bwana Yesu Kristo. Omba ili uwe mwenzi, mzazi, ndugu, mwana/binti kama anavyotaka Yesu uwe.
- **Ombea** Siku ya Maombi ya Ndoa & Familia (Juni 6, 2020) iliyoandaliwa na Idara Huduma za Familia ya Konferensi Kuu. (Tembelea: family.adventist.org) .
- **Ombea** watu wanaoishi peke yao wakijisikia upweke sana hasa wakati huu. Waombee ili waone mibaraka ya kuwa peke yao hasa katika kumtumikia Mungu. Omba kwamba kama ni mapenzi ya Mungu waweze kupata wenzi wacha Mungu.
- **Ombea** watu wanaopambana na uraibu.
- **Ombea** mshiriki wa kanisa kule Trinidad ambaye binti yake aliuawa miaka miwili iliyopita, na kijana wake wa kiume aliuawa mwezi Machi mwaka huu. Mwombee ili apate faraja na pia apate ulinzi kwa familia yake iliyosalia.

Siku ya 55, Jumatano, Mei 20, 2020

KUJITOA KWA KANISA LAKO MAHALIA

Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika – Acts 4:32

"Waongofu wa injili walikuwa na 'moyo mmoja na roho moja.' Shauku moja iliwaongoza wote – mafanikio ya utume ya waliopewa dhamana; tamaa haikuwa na nafasi maishani mwao. Upendo kwa ndugu na kazi waliyokusudia, ulikuwa mkubwa kuliko upendo wao kwa fedha na mali. Kazi zao zilishuhudia kwamba walizihesabu roho za watu kuwa ni za thamani kubwa kuliko utajiri wa kidunia. Ndivyo itakavyokuwa daima Roho wa Mungu anapoyamiliki maisha." – Acts of the Apostles, 70

Maswali ya Moyoni: Kuna nyakati ambapo huwa tunaweza kuchanganyikiwa na kanisa letu mahalia au hata kanisa la ulimwengu. Lakini bado tunajua kuwa kanisa ni mchumba wa Kristo. Ikiwa Yesu amejitoa hivyo kwa kanisa, si inatupasa sisi tujitoe kwake pia? Wakristo wa awali walijazwa na Roho na walikuwa tayari kutoa kafara yote kwa ajili ya kanisa na utume. Kwa nini leo usimwombe Mungu akusamehe kwa ajili ya baadhi ya mitazamo ya dhambi unayoweza kuwa nayo dhidi ya mchumba wake, na kumwomba akubatize kwa ubatizo wa Roho wake, akikupa nguvu za kuutafuta umoja, na kuishi maisha ya kujitoa kafara ili kusaidia na kubariki jumuiya ya kanisa lako mahalia.

Taarifa za Sifa

- Tunamsifu Mungu kwa ajili ya makanisa mapya 900 yaliyoanzishwa katika miaka michache iliyopita katika Divisheni ya Kusini mwa Amerika.
- Katika Divisheni ya Kusini mwa Amerika mahitaji ya watu kujifunza Biblia yameongezeka mara 5 zaidi tangu zahama hii ilipoanza!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** kanisa katika nchi ya Gabon. Ombea washiriki wake wawe na moyo na hekima ya kuwafikia raia wenzao. Kwa namna ya pekee ombea kundi la Akanda ambao wanajaribu kuwahudumia wale wenye ulemavu.
- **Ombea** mahitaji ya kanisa lako mahalia. Ombea umoja, uponyaji na kujitoa upya kwa ajili ya kushuhudia na shughuli za utume.
- **Ombea** wachungaji na viongozi wa kanisa katika baadhi ya maeneo ya Unioni ya Haitia. Ombea kanisa katika baadhi ya maeneo ya Haiti ambayo yamejaa vikundi vya majambazi wenye silaha. Ombea afya ya kiroho, kimwili, kifedha na kiakili ya washiriki wa Haiti.
- Ombea washiriki walioyapokea mafundisho potofu au mtazamo uliogeuzwa na wanajaribu kuwadanganya wengine.
- Ombea washiriki wa zamani waliojitenga na kanisa na kuunda makundi yao au madhehebu yao. Waombee ili waongozwe kwenye ukweli.

Siku ya 56, Alhamisi, Mei 21, 2020

KUJITOA KWA AJILI YA UTUME WA MUNGU

Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu – 1 Kor. 9:19, 22b

"Kila mwanafunzi wa kweli amezaliwa katika ufalme wa Mungu kama Mmishonari" – DA, 195

Maswali ya Moyoni:
Kazi ya Umishonari, uinjilisti, haya sio maeneo ya huduma waliyowekewa wachungaji peke yao au wainjilisti waliofundishwa. Kila mwumini ambaye ndani ya moyo wake Yesu hukaa kwa njia ya Roho, anaitwa kuangaza nuru katika ulimwengu huu kwa njia ya maneno ya kweli na matendo ya upendo. Kwa nini usimwombe Kristo sasa ili akuoneshe eneo lako la utume leo ni nani na ni wapi? Sihi kwa ajili ya huruma ya kweli kwa roho zilizopotea na moyo wa kushiriki imani yako pamoja na upendo kwa watu walio katika eneo lako la ushawishi.

Taarif a za Sifa:

- **Familia ya Makoba**, wanasema, "Siku 100 za Maombi zimekuwa ni uzoefu mzuri kwetu kama familia. Ingawa hali inayotuzunguka inaonekana kuwa ni ya kutisha, kama familia tunakitumia kipindi hiki kuyatoa upya maisha yetu kwa Yesu kwa kuifuatilia programu ya Siku 100 za Maombi kwa umakini."
- Timu ya vijana ya kule Guwahati, India, ilikuwa tayari kuwafikia Wahindu kwa ujumbe wa afya kabla tu ya zuio lililosababishwa na COVID-19

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kuelewa kwamba utume wa Mungu kwa ajili yako ni nini mahali ulipo sasa. Mwombe Mungu akusaidie kuwa mwaminifu katika kumshuhudia Kristo kwa maneno yako, vitendo, na mwenendo kwa watu wanaokuzunguka.
- **Ombea** hospitali zote za Kiadventista kwani zina mahitaji mengi wakati wa zahama hii. Omba kwamba madaktari, wauguzi na wafanyakazi wengine watiwe nguvu na Roho Mtakatifu kuwa washuhudiaji kwa wagonjwa wao.
- **Ombea** vituo vya kanisa viitwavyo 'Life Hope Centers' ulimwenguni kote ili viwe nguzo ya nuru katika siku hizi za giza.
- **Ombea** miji kikubwa katika nchi yako ili Mungu atupatie uwezo wa kuwafikia watu katika maeneo haya.
- **Ombea** wamishonari wa mstari wa mbele, hasa katika dirisha la 10/40 wanaotafuta kumleta Yesu kwenye jumuiya zilizokuwa zikitawaliwa na Shetani kwa maelfu ya miaka.